THE STATE EDUCATION DEPARTMENT /
THE UNIVERSITY OF THE STATE OF NEW YORK / ALBANY, NY 12234

55 Hanson Place, Room 594
Brooklyn, New York 11217
Tel: 718-722-2445 Fax: 718-722-2459

89 Washington Avenue, Room 528EB
Albany, New York 12234
Tel: 518-474-8775 Fax: 518-474-7948

SHERIA ZA HAKI ZA WAZAZI KWA WANAFUNZI WA LUGHA YA KIINGEREZA KATIKA JIMBO LA NEW YORK

Sheria za Kamishna wa Idara ya Elimu ya Jimbo la New York (NYSED) sehemu ya 154 inakupa wewe – mzazi/mlezi wa Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza (ELLs) –:

1. Haki ya watoto wako kupokea elimu ya umma bila malipo katika wilaya ya shule ambayo unaishi, haijalishi hali yako ya uhamiaji au ya watoto wako (k.m., kama wanafamilia wako ni raia, wahamiaji, au wasio halali) na lugha ambayo wewe au watoto wako wanaongea.

2. Haki ya kuwaandikisha watoto wako shuleni bila kuombwa kutoa maelezo au stakabadhi ambazo zinaweza kufichua hali ya uhamiaji ya watoto wako. Huwezi kuombwa utoe kadi au nambari ya ruzuku ya serikali, visa ya uhamiaji au hali ya visa, au stakabadhi za uraia au hali ya uraia.

3. Haki chini ya sheria ya serikali ya kuwa na mkalimani/mtafsiri kwa lugha yako unayopendelea kwa ajili ya mwingiliano muhimu na wilaya ya shule.

4. Haki ya kuwa na watoto wako katika mpango wa Elimu ya Lugha Mbili (Bilingual Education (BE)) wakati kuna wanafunzi 20 au zaidi wa kiwango cha gredi ambao wanaongea lugha moja ya nyumbani/msingi. [1]

5. Haki ya kp(anaong)0ip-11gI4040 /4 nya/oan.5 (z)8(k)-12.9 9 (ai)2.6 (di)2.89 9 (ai11.3 K)iilo cikaianaon(m)-6 (u y)8 (ak)

8. Haki ya kukutana na wahudumu wa shule angalau mara moja kwa mwaka, kwa kuongezea mikutano mingine ya jumla inayohitajika, ili kujadili maendeleo ya jumla ya masomo na lugha ya watoto wako.